

CHANGAMOTO

TOKA

ROMA

KWA NINI WAPROTESTANTI

WANAITUNZA JUMAPILI?

CHANGAMOTO

TOKA

ROMA

=====

Kwa Nini Waprotestanti

Wanaitunza Jumapili?

=====

Kutoka katika Makala za Gazeti la

Catholic Mirror

za mwaka 1893

kuhusu hoja hiyo hap juu

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Rome's Challenge: Why Do Protestants Keep Sunday? - Kiswahili

## DIBAJI

FEBRUARI 24, 1893, Konferensi Kuu (GC) ya Waadventista Wasabato ilipitisha maazimio fulani yaliyoimba Serikali pamoja na watu wa Marekani (U.S.) kutokana na maamuzi ya Mahakama Kuu (Supreme Court) yaliyolitangaza taifa hili [la Marekani] kuwa ni la Kikristo, na kutokana na utendaji wa Bunge la Marekani (Congress) wa kutunga amri inayohusu suala la kidini, na kutoa maneno ya kuizuia kanuni ile pamoja na matokeo yake yote ya kanuni ile. Katika mwezi wa Machi, 1893, Chama cha Kimataifa cha Uhuru wa Dini (International Religious Liberty Association) kilichapisha maazimio hayo katika kijizuu chenye kichwa cha Lalamiko na Maneno ya Kuizuia Amri Iliyotolewa (Appeal and Remonstrance). Baada ya kupokea kimojawapo cha [vijizuu] hivyo, Mhariri wa gazeti la Catholic Mirror la [mji wa] Baltimore, Maryland, alichapisha mfululizo wa maoni manne yaliyotolewa na Mhariri huyo ambayo yalitokea katika gazeti lile tarehe 2, 9, 16, na 23 ya mwezi wa Septemba, 1893. Gazeti hilo la Catholic Mirror lilikuwa chombo rasmi cha Kadinali Gibbons pamoja na Upapa katika nchi hii ya Marekani (U.S.). Kwa hiyo, ingawa makala

hizo hazikuandikwa kwa mkono wake mwenyewe Kadinali huyo, zilitolewa chini ya idhini ya Ofisi yake, na kuwa kama usemi uliotolewa na Upapa juu ya somo hilo, ambazo zimekuwa changamoto ya wazi toka kwa Upapa dhidi ya Uprotestanti, pamoja na madai yatokayo kwa Upapa huo kuwataka Waprotestanti watoe jibu lao kwa Upapa kwa nini wao wanaitunza Jumapili na pia jinsi wanavyoitunza.

Suala lifuatalo (ukiondoa maelezo yaliyoandikwa chini ya [mwisho wa] ukurasa, na maelezo ya mhariri wetu katika mibano hii [ ] kuanzia ukurasa wa 20 na kuishia ukurasa wa 21, pamoja na Nyongeza zile mbili) ni uchapishaji uliorudiwa tena wa neno kwa neno wa uhariri huo [wa gazeti la Catholic Mirror], pamoja na kichwa cha maneno kinachoonekana katika ukurasa wa 4.

SABATO YA KIKRISTO

MTOTO HALALI WA MUUNGANO WA ROHO MTAKATIFU

NA KANISA KATOLIKI AMBALO NI BIBI-ARUSI WAKE.

MADAI YA WAPROTESTANTI KATIKA KIPENGELE

CHO CHOTE NDANI YAKE YAMETHIBITISHWA

KUWA HAYANA MSINGI, YANAJIKANUSHA

YENYEWE NA KUJIFISHA YENYEWE

---

[Toka katika Gazeti la Catholic Mirror la Sept. 2, 1893.]

Mawazo yetu yamevutwa kuliangalia somo hilo hapo juu katika juma lile lililopita kwa njia ya kupokea kijizuu cha kurasa ishirini na moja, kilichochapishwa na Chama cha Kimataifa cha Uhuru wa Dini, kilichokuwa na kichwa cha "Lalamiko na Kuizuia Amri Iliyotolewa," ambacho kina maazimio yaliyopitishwa na Konferensi Kuu (GC) ya Waadventista Wasabato (Feb. 24, 1893). Maazimio hayo yanakosoa na kutoa lawama, kwa ukali mwingi, dhidi ya kitendo cha Bunge la Marekani (U.S. Congress), na kile cha Mahakama Kuu (Supreme Court), kuingilia haki za watu kwa kufunga Sikukuu ya Ulimwengu ya Tamasha na Kuuza Vitu (World's Fair) siku ya Jumapili.

Waadventista ndilo kundi la pekee la Wakristo ambalo linaitegemea Biblia kama mwalimu wao, ambao katika kurasa zake hawaoni amri yo yote inayoruhusu badiliko la siku kutoka ile ya saba kwenda ile ya kwanza. Hivyo wanaitwa jina lao, "Waadventista wa Siku ya Saba (Seventh-day Adventists)." Kanuni yao kuu inahusu kuitenga Jumamosi kwa ajili ya ibada ya Mungu peke yake, kwa kuitii amri hai ya Mungu mwenyewe, ambayo imerudiwa tena na tena katika vitabu vile vitakatifu vya Agano la Kale na Agano Jipya, ambayo wana wa Israeli waliitii neno kwa neno kwa

maelfu ya miaka mpaka hivi leo, na kuungwa mkono na mafundisho na desturi ya Mwana wa Mungu alipokuwa hapa duniani.

Kinyume chake, Waprotestanti wa Ulimwengu Mzima, ukiwaondoa hao Waadventista [Wasabato], wakiwa na Biblia ile ile kama mwalimu wao anayependwa kwa dhati na ambaye peke yake hawezi kukosea, kwa desturi yao, tangu kutokea kwao katika karne ile ya kumi na sita, mbele ya macho yao wakiwa na desturi ile iliyoheshimiwa sana na Wayahudi kwa kipindi kirefu, wameikataa katakata siku ya ibada iliyotajwa kwa jina lake [Sabato], na kwa kinyume dhahiri na amri yake, kutwaa siku ya ibada ya kumwabudu yeye ambayo haikupata kutajwa kamwe kwa kusudi hilo katika kurasa za Gombo hilo Takatifu [Biblia].

Ni mimbara gani ya Kiprotestanti ambayo karibu kila siku ya Jumapili haipigi makelele na kutoa shutuma kali kwa ghadhabu dhidi ya kuinajisi Sabato [Jumapili]? Ni nani awezaye kusahau makelele ya kinafiki ya wachungaji wa Kiprotestanti kupinga ufunguaji wa milango siku hiyo ya Jumapili kwa ajili ya Sikukuu ya Ulimwengu ya Tamasha na Kuuza Vitu (World's Fair)? na yale maelfu ya malalamiko yaliyotiwa sahihi na mamilioni ya watu ili kuiokoa Siku ya Bwana [Jumapili] isinajisiwe? Hakika, msisimko huo wa watu wengi ulioenea mahali pengi na upingaji huo uliojaa makelele usingeweza kuwako bila kuwa na sababu zenye nguvu sana kwa upi nzani huo wenye nguvu.

Na wakati ule maeneo yalipogawiwa kwa madhehebu mbalimbali za Kiprotestanti katika [eneo] la Sikukuu ile ya Ulimwengu ya Tamasha na Kuuza Vitu ili wapate kuonyesha vitu vyao, ni nani awezaye kusahau maneno yao ya uadilifu na kukataa kufanya mambo hayo kwa kuwa yanakwenda kinyume na dini yao ambayo yalitolewa na ndugu zetu Wapresibiteri (Presbyterians), mara tu walipojua habari ya maamuzi yaliyotolewa na Mahakama yetu Kuu kutoingilia kati katika ufunguzi [wa Sikukuu hiyo] siku ya Jumapili? Magazeti yalitupasha habari kuwa walikataa katakata kulitumia eneo walilopewa, au kufungua masanduku yao, wakidai kuwa wanayo haki ya kuviondoa vitu vyao kutokana na kuzishikilia kanuni zao kwa ushupavu, na hivyo kukataa kwamba hawana uhusiano wo wote na Maonyesho hayo yanayokufuru na kuivunja Sabato hiyo [Jumapili].

Bila shaka, ndugu zetu Wakalvini (Calvinists) walihusika, tena waliunga mkono madhehebu zote nyingine ambazo, hata hivyo, zilipoteza maeneo yao ya kusimama na kujionyesha kana kwamba wao ni wafia dini kwa kutetea utunzaji wa Sabato hiyo [Jumapili].

Hivyo wao wakawa "tamasha kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu," ingawa ndugu zao wa Kiprotestanti waliokosa kushiriki katika biashara hiyo, bila upendo na kwa wivu walionyeshwa kuwa ushupavu wao wa kanuni yao hiyo ya dini ulitokana na kiburi chao cha Kifarisayo na ukaidi wao sugu.

Madhumuni yetu ya kutoa makala hii ni kutoa nuru kama ile itakayowawezesha wasomaji wetu kuielewa hoja hii kwa mapana yake yote na kwa njia hiyo kuifikia imani halisi juu ya hoja hii ya maana sana (kwa maana hoja hii juu ya Sabato [Jumapili] kama ingeondolewa isihubiriwe katika mimbara za Kiprotestanti, basi, madhehebu hizo zingejihisi kuwa zimepotea, na wahubiri wake wangepoteza "kitumbua chao [Jibini yao toka Cheshire]").

Ulimwengu wa Kikristo, tukisema kimaadili, umekuwa na msimamo mmoja juu ya hoja hiyo na desturi ya kumwabudu Mungu katika siku hiyo ya kwanza ya juma [Jumapili].

Waisraeli, waliotawanyika ulimwenguni kote, wanaitunza siku ya mwisho ya juma [Jumamosi] kama siku takatifu ya kumwabudu Mungu. Katika suala hilo, Waadventista Wasabato (dhehebu la Wakristo lenye watu wachache mno) wamechagua pia siku iyo hiyo [Jumamosi].

Waisraeli na Waadventista wote wanaitumia Biblia kuitetea amri hiyo ya Mungu, wakiendelea kuitunza kwa makini sana Jumamosi hiyo.

Waisraeli wanaheshimu mamlaka ya Agano la Kale peke yake, lakini Mwaadventista, ambaye ni Mkristo, analikubali Agano Jipya kwa msingi ule ule kama lile la Kale, yaani, kuwa ni kumbukumbu iliyovuviwa pia. Yeye anaona kwamba Biblia, mwalimu wake, inakubaliana katika sehemu zake hizo mbili, kwamba Mkombozi, wakati ule alipokuwa hai, kamwe hakuitunza siku nyingine yo yote zaidi ya ile ya Jumamosi. Injili zinaonyesha waziwazi ukweli huo kumhusu yeye [Kristo]; wakati, katika kurasa za kitabu cha Matendo ya Mitume, Nyaraka, na Ufunuo, haipatikani amri yo yote inayoifuta Jumamosi iliyowekwa.

Kwa hiyo, Waadventista wakiwa na msimamo mmoja na Waisraeli, wanapata imani yao hiyo kutoka katika Agano la Kale, msimamo ambao unathibitishwa na mafundisho ya Neno takatifu kwa maisha na desturi hiyo ya Mkombozi pamoja na Mitume wale kwa karibu karne moja [miaka ile mia moja ya mwanzo] ya kipindi kile cha Ukristo.

Tukifikiria kitakwimu, Waadventista Wasabato ni seemu ndogo mno ya Waprotestanti wote ulimwenguni, lakini, kwa vile hoja hii sio juu ya wingi wa watu, bali ni juu ya ile kweli, na haki, hapo hisia kali ya kutenda haki inatukataza kulishutumumu dhehebu hilo dogo bila kuwa na uchunguzi uliofanywa kwa utulivu, na ule usiopendelea upande wo wote; hayo si mazishi yanayotuhusu sisi.

Ulimwengu wa Kiprotestanti, tangu kuzaliwa kwake katika karne ile ya kumi na sita, umeafikiana kabisa na Kanisa Katoliki katika "kuitakasa" sio Jumamosi, bali Jumapili. Mjadala juu ya sababu zilizoleta hisia hiyo ya aina moja na desturi hiyo [ya kuitunza Jumapili] kwa zaidi ya miaka 300 [kabla ya 1893], zitaaisaidia katika kuuweka Uprotestanti juu ya msingi imara katika suala hili, endapo sababu zilizotolewa kuunga mkono msimamo wake huo zitazishinda zile zilizotolewa na Wayahudi na Waadventista [Wasabato], Biblia, mwalimu pekee anayetambuliwa na wadai hao wote wawili, akiwa ndiye mwamuzi wetu na shahidi. Walakini, kwa upande mwingine, kama hao wa mwisho watatoa sababu zisizoweza kukanushwa na umati mkubwa wa Waprotestanti, basi, makundi hayo mawili ya wadai hao yanayomtaja mwalimu wao huyo, yaani, Biblia, kundi kubwa la Waprotestanti, mbali na kupiga makelele yao, kama wanavyofanya kwa kuitunza Jumapili kwa ukali, hawana njia yo yote nyingine ya kufuata kuliko ile ya kukubali kuwa wamekuwa wakifundisha na kuifuata desturi potofu kimaandiko kwa zaidi ya karne tatu [kufikia 1893], kwa kutumia mafundisho na desturi za kanisa lile lililoasi [Kanisa Katoliki] kama walivyoamini kinafiki sikuzote, kinyume cha kila idhini na mafundisho ya Maandiko Matakatifu. Kuongezea juu ya kosa hilo zito [kubwa] la Kimaandiko, lisilosameheka, suala hilo linahusu moja wapo ya amri hai, yenye nguvu ya Mungu kwa mtumishi wake, yaani, kwa mwanadamu, isemayo: "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase."



Hakuna Mprotestanti ye yote aliye hai leo ambaye mpaka sasa amepata kuitii amri ile, akiwa anapendelea kulifuata Kanisa lililoasi lililokwisha kutajwa kuliko kumfuata mwalimu wake, yaani, Biblia, ambayo, toka Mwanzo hadi Ufunuo, haifundishi fundisho [tofauti] jingine lo lote la dini, endapo Waisraeli na Waadventista Wasabato watakuwa sahihi. Pande zote mbili zinaitumia Biblia kama mwalimu wao "asiyeweza kukosea kamwe." Hebu na tuiache Biblia iamue kama Jumamosi au Jumapili ndiyo siku ile iliyoamriwa na Mungu. Mojawapo ya makundi hayo mawili ni lazima limekosea, na, wakati msimamo potofu juu ya hoja hii ya maana sana unaambatana na adhabu ya kutisha sana, iliyotishiwa na Mungu mwenyewe dhidi ya yule atakayelivunja hilo "agano la milele [Sabato]," tutaingia katika mjadala wetu kuona kama sababu zilizotolewa na pande zote mbili zinafaa. Wala mjadala huo wa somo hili kuu haupiti uwezo wa mawazo ya wanadamu wa kawaida, wala hauhitaji utafiti usiokuwa wa kawaida. Lenyewe linasulihishwa kwa njia ya maswali machache yaliyo wazi ambayo ni rahisi kuyatataua:

Kwanza. Ni siku gani ya juma ambayo Biblia inaamuru itakaswe?

Pili. Je, Agano Jipya limeibadili kidogo amri ile ya awali na kuweka amri ama desturi nyingine mpya?

Tatu. Je, Waprotestanti, tangu karne ile ya kumi na sita, wameitii amri ya Mungu kwa "kuitakasa" siku ile iliyoamriwa na kiongozi na mwalimu wao yule asiyekosea kamwe, yaani, Biblia? na kama jibu ni hapana, kwa nini wasifanye hivyo?

Kwa maswali hayo matatu yaliyotajwa hapo juu sisi wenyewe tunatoa ahadi ya kuwapa majibu mengi ya busara, ambayo hayawezi kushindwa kuitetea kweli na kuthibitisha mageuzi mabaya ya kosa [fundisho potofu] hilo [yaliyokwisha kufanywa].

[Toka katika gazeti la Catholic Mirror la Sept. 9, 1893.]

"Lakini imani, imani ile shupavu isiyotumia akili,

Mara tu inapounganishwa upesi na uongo fulani

unaopendeza sana, inaukumbatia mpaka mwisho."

----- Moore.

Kufuatana na ahadi yetu tuliyotoa katika toleo letu lililopita, tunasonga mbele na kulifichua mojawapo ya makosa [mafundisho potofu] mabaya sana na mageuzi yasiyosameheka kabisa ya kanuni ile ya Biblia juu ya imani. Walakini, ili tusije tukaeleweka vibaya, tunafikiri kwamba ni muhimu kutanguliza hoja isemayo kwamba Uprotestanti hautambui kanuni yo yote ya imani, mwalimu ye yote, isipokuwa tu ile "Biblia isiyoweza kukosea kamwe." Kama vile Mkatoliki anavyoyatupilia mbali maamuzi yake yote katika mambo ya kiroho, na kwa imani isiyo na masharti anaitii sauti ya Kanisa lake, hivyo ndivyo Mprotestanti pia asivyoweza kumtambua mwalimu mwingine ye yote isipokuwa Biblia peke yake. Maisha yake yote ya kiroho yanatokana na mafundisho yake [Biblia]. Ni kwake sauti ya Mungu inazungumza naye kwa njia ya mwalimu wake huyo wa pekee aliyevuviwa [Biblia]. Anayo dini yake yote, imani yake yote, na desturi zake zote. Lugha ya Chillingworth, isemayo, "Biblia, Biblia nzima, si kitu kingine cho chote ila Biblia peke yake, hiyo ndiyo dini ya Waprotestanti," ni mfano tu wa wazo lile lile lililogeuzwa kwa namna mbalimbali katika mifano mingine, kama vile, "Kitabu cha Mungu," "Mkataba wa Wokovu Wetu," "Mausia ya Imani Yetu ya Kikristo," "Kitabu cha Mungu cha Mafundisho kwa taifa la Wanadamu," n.k., n.k. Basi, ni ukweli usiokanushika kwamba Biblia peke yake ndiye mwalimu wa Ukristo ule wa Kiprotestanti. Tukiuzingatia ukweli huo,basi,sasa tunaweza kuendelea kujadili ustahili wa hoja iliyohusika katika toleo letu lililopita.

Tukiwa tunakitambua kile kisichoweza kukanushwa, ukweli wa tofauti ya moja kwa moja kati ya mafundisho na desturi za Ukristo ule wa Kiprotestanti ----- ukiwaondoa Waadventista Wasabato --- -- kwa upande mmoja, na [mafundisho] yale ya Wayahudi kwa upande mwingine, wote wakiwa wanaadhimisha siku tofauti za juma, tutaendelea kuchukua ushuhuda kutoka kwa shahidi peke yake anayeweza kupatikana katika hoja hizo [mbili]: yaani, ushuhuda wa mwalimu yule anayejulikana sana kwa wadai wote wawili, yaani, Biblia. Usemi wa kwanza tunaokutana nao katika Neno hilo Takatifu unapatikana katika Mwanzo 2:2: "Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya." Kumbukumbu inayofuata katika suala hili inapatikana katika Kutoka 20, ambapo Mungu aliamuru siku ya saba itunzwe, kwa sababu alitaka itunzwe, akasema maneno yafuatayo: "Kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa." Tena, twasoma katika sura ile ya 31 fungu la 15 maneno haya: "Kazi itafanywa kwa siku sita; lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe [kupumzika] kabisa, takatifu kwa BWANA." fungu la kumi na sita lasema hivi: "Ni agano la milele," "ni ishara [ya] ... milele," "kwani kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika."

Katika Agano la Kale Sabato imetajwa mara mia moja na ishirini na sita, na mafungu yote hayo yanatoa shauri moja linalopatana yakitangaza mapenzi yake Mungu katika kuiamuru siku ya saba ipate kutunzwa, kwa sababu Mungu mwenyewe ndiye aliyeitunza kwanza, akiifanya iwafunge wote kama "agano la milele." Wala hatuwezi kuwaza kwamba mtu ye yote anaweza kuwa mwenda wazimu kiasi cha kuitilia mashaka siku ya Jumamosi kuwa siyo Sabato ile ile au siku ya saba ile ile [ya kwanza], kwa kuwaona Waisraeli ya kuwa wamekuwa wakiitunza siku ya Jumamosi tangu Sheria ile [Amri Kumi] ilipotolewa kwao [Mlimani Sinai], mwaka ule wa 2514 toka Mwanzo (A.M.) hadi mwaka wa 1893 B.K., kipindi cha miaka ipatayo 3383. Tukiwa na kielelezo cha

Waisraeli mbele ya macho yetu leo, hakuna ukweli wo wote wa kihistoria uliohibitika vizuri sana kuliko huo uliokwisha kutajwa; yaani, kwamba watu wa Mungu wateule, walinzi [wadhamini] wa Agano la Kale, wawakilishi hai wa dini pekee ya Mungu toka zamani mpaka sasa, kwa miaka 1490 kabla ya Ukristo kuja walikuwa wameitunza desturi hiyo ya kila juma yakiwa ni mapokeo hai ya tafsiri sahihi ya siku hiyo ya pekee ya juma, yaani, Jumamosi, na kuitunza kama "takatifu kwa BWANA," mapokeo ambayo wameendelea nayo kwa desturi yao kwa kipindi kingine zaidi cha miaka 1893, hivyo wakikifunika kipindi kamili cha Ukristo. Tunaona kwamba ni lazima kuwa wazi kabisa katika jambo hili, kwa sababu zile zitakazojidhihirisha kikamilifu kuanzia hapa. Biblia ----- Agano la Kale ----- ikithibitishwa na mapokeo hai ya desturi hiyo ya kila juma [ya kupumzika Jumamosi] iliyoifanywa na wateule wake Mungu kwa miaka hiyo 3383, basi, hutufundisha kwa uhakika kamili, kwamba Mungu mwenyewe, alikuwa ameitaja kwa jina siku ile iliyoipaswa kutunzwa "takatifu kwake," ----- kwamba siku ile ilikuwa ni Jumamosi, na ya kwamba uvunjaji wo wote wa amri ile uliadhibiwa kwa kifo. "Basi mtaishika hiyo Sabato [Jumamosi]; kwa kuwa ni takatifu kwenu; kila mtu atakayeitia unajisi [atakayeivunja] hakika yake atauawa; kwa kuwa kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo, nafsi hiyo itakatiliwa mbali na watu wake." Kutoka 31:14.

Ni vigumu kabisa kutekeleza adhabu kali zaidi ya hiyo iliyotamkwa na Mungu mwenyewe katika fungu hilo hapo juu kwa wote wanaoivunja amri hiyo ambayo imetajwa si chini ya mara mia moja na ishirini na sita katika torati ile ya zamani. Amri zile Kumi za Agano la Kale kwa desturi zinapigwa chapa katika kumbukumbu ya mtoto wa Mkristo anayefuata Biblia mapema iwezekanavyo, lakini hakuna amri moja katika hizo kumi ambayo inajulikana sana katika Shule ya Jumapili na mimbarani kama ile ya "kuitakasa" siku ya Sabato.

Baada ya kuhakikisha kabisa mapenzi ya Mungu kuhusu siku ile inayopaswa kutakaswa kutoka katika Neno lake Takatifu, kwa sababu alistarehe siku ile, yaani, siku ile inayothibitishwa kwetu kwa desturi ya watu wale walioteuliwa na Mungu [Waisraeli] kwa maelfu ya miaka, tunashawishiwa kwa kawaida kuuliza ni lini na wapi Mungu alipoibariki siku ya ibada yake; kwa maana ni dhahiri kwa ulimwengu mzima kuwa badiliko la siku limetokea, na kwa vile hakuna kidokezo cho chote cha badiliko hilo kinachoweza kupatikana ndani ya kurasa za Agano la Kale, wala katika desturi ya Wayahudi ambao wanaendelea kwa karibu karne kumi na tisa za Ukristo [kufikia 1893] kuitii amri ile iliyoandikwa, basi, hatuna budi kumwalia mtoa habari za kipindi kile cha Ukristo; yaani, Agano Jipya, ili kuona amri ya Mungu inayoifutilia mbali Sabato lile ya zamani; yaani, Jumamosi.

Sasa tunakikaribia kipindi kile kinachofunika muda mfupi wa karne kumi na tisa, na kuendelea kuchunguza kama mwalimu huyo wa ziada atokaye mbinguni ----- Agano Jipya ----- anayo amri inayofuta mamlaka ya amri ile ya zamani [Jumamosi], na, kwa wakati uo huo, kuweka siku [nyingine] badala ya Sabato ile iliyowekwa na Mungu katika Sheria ile ya zamani [Amri Kumi], yaani, Jumamosi; maana, kwa vile Jumamosi ilikuwa ndiyo siku iliyotunzwa na kuamriwa kutunzwa na Mungu, basi, ni mamlaka ya Mungu peke yake, chini ya utaratibu wa amri ya kuibatilisha [kuifuta], ambayo yangeweza kulitangua [kulifuta] agano la [milele] la Jumamosi, na kuweka amri nyingine ya Mungu, inayoitaja siku nyingine kwa jina ili ipate "kutakaswa," mbali na ile ya Jumamosi, ingekuwa ya muhimu kutolewa ili kuiridhisha dhamiri ya muumini Mkristo. Biblia akiwa ndiye mwalimu pekee anayetambuliwa na Mkristo yule anayefuata Biblia, Agano la Kale likiwa limeshindwa kuonyesha badiliko la siku hiyo, wakati uo huo siku nyingine mbali na Jumamosi ikiwa inaendelea "kutakaswa" na ulimwengu ule unaoifuata Biblia, basi, Mkristo yule

aliyefanya matengenezo hayo hakika anawajibika kuonyesha katika kurasa za Agano Jipya amri mpya ya Mungu inayoifuta ile ya Jumamosi na kuiweka ile ya Jumapili, ambayo imetunzwa na wale wanaoifuata Biblia tangu mapambazuko yale ya Matengenezo ya Kanisa (Reformation).

Tunapolikagua kwa makini sana Agano Jipya toka jalada la kwanza hadi jalada la mwisho, tunaona Sabato [Jumamosi] ikitajwa mara sitini. Pia tunamwona Mwokozi sikuzote bila kugeuka alichagua Sabato [Jumamosi] kufundisha katika masinagogi na kufanya miujiza yake. Injili zote nne zinaitaja Sabato (Jumamosi) mara hamsini na moja.

Katika tukio moja Mkombozi huyo anajitaja mwenyewe kuwa yeye ndiye "Bwana wa Sabato [Jumamosi]," kama vile ilivyotajwa na Mathayo na Luka [1], lakini katika kumbukumbu iliyoandikwa juu ya maisha yake, wakati ule, bila kugeuka, alipoitunza na kuitumia siku hiyo (Jumamosi), kamwe hakudokeza hata mara moja kuwa alikuwa na nia ya kuibadili (siku hiyo). Mitume wake pamoja na rafiki zake wanatupatia kielelezo chao kinachotushangaza kuhusu umakini wao [uangalifu wao mkubwa] katika kuitunza [siku hiyo] baada ya kifo chake, na, wakati mwili wake ukingali kaburini, Luka (23:56) anatuambia hivi: "Wakarudi, wakafanya tayari manukato na marhamu. Na siku ya Sabato [Jumamosi] walistarehe kama ilivyoamriwa [Kut. 20:8-11]." "Hata siku ya kwanza ya juma [Jumapili], ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini [sio kanisani kuabudu], wakiyaleta manukato waliyoyaweka tayari [Luka 24:1]. "Manukato" na "marhamu" yale yalikuwa yametayarishwa jioni ya Ijumaa ile Kuu, kwa sababu "Sabato ikaanza kuingia." Fungu la 54. Kitendo hicho kwa upande wa rafiki zake Mwokozi kinathibitisha bila kupingwa kwamba baada ya kifo chake wali"itakasa" Jumamosi ile, na kuiona Jumapili kama siku nyingine yo yote ya kawaida [ya kazi] ya juma. Basi, je! kuna kitu kingine cho chote kinachoweza kuihitimisha hoja hii kuliko kusema kwamba mitume na wanawake wale watakatifu hawakuijua kamwe Sabato nyingine yo yote isipokuwa Jumamosi tu mpaka kufikia siku ile ya kufa kwake Kristo?

Sasa tunaukaribia utafiti wetu wa hoja hii ya kuvutia sana kwa miaka thelathini iliyofuata [baada ya ufufuo wa Kristo], kama ilivyosimuliwa na mwinjilisti Luka katika kitabu chake cha Matendo ya Mitume. Bila shaka dalili fulani ya amri ya kutangua [kufuta Jumamosi] inaweza kugunduliwa katika desturi ya mitume hao katika kipindi kile kirefu.

Lakini, ole wetu! [kwa maana] tunakabiliwa tena na kukatishwa tamaa. Mara tisa [2] tunaikuta Sabato ikitajwa katika kitabu hicho cha Matendo, lakini hiyo ni Jumamosi (yaani, Sabato ile ya zamani). Endapo wasomaji wetu wanataka ushahidi, basi, tunawaelekeza kwenye sura inayohusika pamoja na fungu katika kila mfano tunaoutoa. Matendo 13:14,27,42,44. Mara moja tena, Matendo 15:21; tena, Matendo 16:13; 17:2; 18:4. "Akatoa hoja zake katika sinagogi kila Sabato [Jumamosi], akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani." Hivyo ni Sabato (Jumamosi) [tupu] toka kitabu cha Mwanzo hadi kile cha Ufunuo!!! Vivyo hivyo, ni vigumu kabisa kuona katika Agano Jipya Mwokozi au mitume wake wakiikatiza [wakiizuia isitunzwe] Sabato ile Asilia [Jumamosi], lakini kinyume chake, wanakubaliana kabisa na mpango ule wa awali, naam, iliungwa mkono naye kabisa alipokuwa angali hai; na mitume nao walishiriki kwa vitendo bila kugeuka katika utunzaji wa siku ile [ya Jumamosi], wala sio siku nyingine yo yote, kwa miaka thelathini iliyofuata baada ya kifo chake, kama kilivyotushuhudia kwa utoshelevu kitabu hicho cha Matendo ya Mitume.

Hivyo hitimisho lake [hoja hii] haliepukiki; yaani, kwamba kwa habari ya wale wanaoifuata Biblia kama kiongozi wao, yaani, Waisraeli na Waadventista Wasabato (Seventh-day Adventists) wanao uzito wa pekee wa ushahidi unaowaunga mkono kwa upande wao, ambapo Mprotestanti yule anayeifuata Biblia hana neno hata moja la kujihami kwa kuiweka kwake Jumapili mahali pa Jumamosi. Mengi zaidi utayapata halafu kidogo [yaani, katika makala nyingine itakayotolewa baada ya muda mfupi ujao].

---

Maelezo Chini ya Ukurasa Nyuma

[1] Imetajwa pia katika Marko 2:28. ----- Mhariri.

[2] Ingesomeka nane badala ya tisa. ----- Mhariri.

---

[Toka Katika Gazeti la Catholic Mirror la Sept. 16, 1893.]

Yule mfalme Shetani, aliyekuwa "mwuaji tangu mwanzo," "na baba wa huo (uongo) [Yohana 8:44]," alipochukua jukumu la kuyafumbua macho ya mama yetu yule wa kwanza, Hawa, kwa kuiamsha tamaa yake ya kutaka makuu, alisema, "Nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya," tendo lake hilo lilikuwa la kwanza tu miongoni mwa juhudi zake zinazowashawishi watu na kufanikiwa sana alizozitumia baadaye katika kuwadanganya mamilioni ya watoto wake [Hawa]. Wao, kama vile Hawa, wakiwa wamechelewa mno, wanajifunza thamani ya vishawishi anavyotoa [Shetani] ili kuwavuta kwa werevu wake mbali na utii wao kwa Mungu, lo! ni majuto yalioje hayo! Wala kiini cha somo la mjadala huu sio tofauti na mbinu za kawaida anazotumia mfalme huyo mweusi [yaani, wa giza].

Kwa zaidi ya karne tatu [kufikia 1893] tangu wakati ule [wa Matengenezo ya Kanisa, Shetani] alionyesha mbele ya Wakristo wengi walio na moyo usioridhika na wenye kutaka makuu, matarajio ya kuzindua "njia mpya ya kutokea," kwa kuliacha Kanisa lililoanzishwa na Mwana wa Mungu [Kanisa Katoliki], kama mwalimu wao, na kumchukua mwalimu mpya ----- yaani, Biblia peke yake ----- kama ndiyo mausia ya Mungu yenye nguvu.

Hekima ya yule mwovu iliona mapema mafanikio makubwa ya mbinu hiyo. Wala matokeo yake hayakushindwa kuyafikia matarajio yake ya kuwafisha [kiroho] watu wengi.

Moyo pekee wa ujasiri na kujihatarisha ulihitajika ili kuweza kuongoza katika safari hiyo. Shetani alimpata mtu huyo katika mtawa aliyeasi, Luther, ambaye tena na tena anathibitisha yeye mwenyewe uhusiano ule wa karibu sana uliokuwapo kati ya bwana wake [Shetani] na yeye mwenyewe katika "Mazungumzo yake ya Mezani," pamoja na kazi zake nyingine zilizochapishwa mwaka 1558 pale Wittenberg, chini ya ukaguzi wa Melancthon. Mazungumzo yake na Shetani yaliyofanyika kwa nyakati mbalimbali, yanashuhudiwa na Luther mwenyewe ----- ni shahidi anayestahili kuaminiwa kabisa. Njia ile ya yule nyoka iliyofanikiwa sana mle Bustanini, ndiyo aliyoitumia Luther na kufanikiwa katika Ulimwengu wa Kikristo [1].

"Wape rubani kuiongoza miguu yao inayotangatanga,

Yule aliye jasiri katika hila yake, na aliyefundishwa kudanganya;

Ambaye mkono wake kwa ujasiri utaugeuzia kubaya usukani wake,

Kuelekea pwani zile za maadui, au 'kuwazamisha kabisa chini ya wimbi."

Mwisho uliopendekezwa kwake na yule mwovu katika kulishambulia Kanisa la Kristo [yaani, Kanisa Katoliki] ulikuwa ni maangamizi ya Ukristo, ambao hivi sasa tunaushughulikia ili kuweza kuzichuja njia alizozitumia kuhakikisha mafanikio yake katika jambo hilo. Mpaka sasa, zimeonekana kuwa zinapotosha, zinajipinga zenyewe, na zina makosa. Hivi sasa tutaendelea na uchunguzi zaidi dhidi ya laghai huyo [Luther].

Baada ya kuthibitisha kwa kuonyesha kwamba Mkombozi, kwa hali yo yote ile, katika kipindi cha maisha yake, hakukosa kuitunza Sabato (Jumamosi) kwa uaminifu, ambayo imetajwa na wainjilisti wale wanne mara hamsini na moja, ingawa yeye mwenyewe alikuwa amejijita "Bwana wa Sabato

[Jumamosi]," kamwe hakupata hata mara moja, kwa kutoa amri au kwa mazoea yake, kudokeza shauku kwa upande wake ya kuibadili siku ile kwa kuweka siku nyingine mahali pake, na baada ya sisi kuwaelekeza mawazo yenu ya pekee kuangalia mwenendo wa wale mitume wake na wanawake wale watakatifu, jioni ile ile ya kifo chake, wakinunua mapema manukato na marhamu yatakayotumika kuupaka mwili wake asubuhi ile baada ya Sabato (Jumamosi), kama Mtakatifu Luka anavyotueleza waziwazi (Luka 24:1), hivyo kwa nasibu, kitendo kile cha Mungu na mapenzi ya Mwana wa Mungu katika maisha yake yote, wakakwepa kukivuruga kwa kuitunza Sabato (Jumamosi) ile kwa makini; tena tukiwa tumekwisha kuyaelekeza mawazo yenu kwenye kitendo kile cha wawakilishi wake hai [cha kuitunza Sabato (Jumamosi)] baada ya kifo chake, kama ilivyothibitishwa na Mtakatifu Luka; pia tukiwa tumekwisha kuweka mbele ya wasomaji wetu ukweli ule usiokanushika unaoonyesha kwamba wale mitume kwa miaka thelathini iliyofuata [baada ya kifo chake Kristo], (angalia Matendo ya Mitume), hawakuweza kamwe kuiacha desturi hiyo ya Bwana wao wa Kimbingu katika kufuata mfano huo, kama Mtakatifu Luka (Matendo 18:4) anavyotuhakikishia sisi, akisema: "Akatoa (yule Paulo) hoja zake katika sinagogi kila Sabato (Jumamosi), akajaribu kuwavuta Wayahudi na Wayunani" kwa pamoja.

Pia tukiwa tumeyaelekeza mawazo yenu kwenye mafungu yale katika kitabu cha Matendo kuhusu matumizi ya pekee ya Sabato (Jumamosi) kwa Wayahudi na Wakristo kwa miaka thelathini baada ya kifo cha Mwokozi kuwa hiyo ndiyo siku peke yake ya juma iliyotunzwa na Kristo na Mitume wake, katika kipindi kile kinachofikia mwisho wa kumbukumbu yote iliyovuviwa, basi, sasa tunaendelea kuongezea juu ya ushahidi wetu tuliotoa kuwa Sabato (Jumamosi) ilikuwa na fursa hiyo ya pekee, kwa kuwakumbusha ninyi kila mfano ambao kumbukumbu hiyo takatifu inaitaja siku ya kwanza ya juma [Jumapili].

Kuitaja Jumapili kwa mara ya kwanza baada ya ufufuo wa Kristo tunakupata katika Injili ya Mtakatifu Luka, sura ya 24, mafungu ya 33-40, na katika Mtakatifu Yohana 20:19. Mafungu hayo juu yanaeleza yenyewe kusudi moja tu la mkutano ule kwa upande wa mitume. Ulitokea siku ile ya ufufuo (Jumapili ya Pasaka), sio kwa kusudi la kuzindua "badiliko jipya lililoacha njia" kutoka Sabato ile ya zamani (Jumamosi) na kui"takasa" siku ile mpya [Jumapili], kwa maana hakuna kidokezo hata kimoja cha kuwapo kwa sala, maonyo, au kusoma Maandiko [siku ile ya Jumapili], ila inaonyesha tu hali ya kuvunjika moyo kabisa waliyokuwa nayo wale mitume kwa kuwajulisha wanadamu kuwa walikuwa wamesongamana pamoja katika chumba kile kule Yerusalemu "kwa hofu ya Wayahudi," kama Mtakatifu Yohana tuliyemnukuu hapo juu anavyotupasha habari hizo kwa wazi.

Kutajwa kwa mara ya pili kwa Jumapili kunapatikana katika Injili ya Mtakatifu Yohana, sura ya 20, fungu la 26 hadi la 29: "Basi, baada ya siku nane, wanafunzi wake walikuwamo ndani tena, na Tomaso pamoja nao." Mkombozi yule aliyefufuka alichukua fursa hii ya kuonana na mkutano wa mitume wote ili kumfedhehesha Tomaso kwa kutokuamini kwake, ambaye alikuwa hayupo katika mkutano ule wa jioni wa Sikukuu ile ya Pasaka. Jambo hilo lingekuwa limempatia nafasi nzuri sana Mkombozi yule kuweza kuibadili siku hiyo mbele ya mitume wake wote, lakini sisi tunasema ukweli ule wa kawaida kwamba, katika tukio hili, kama katika siku ile ya Pasaka, hakuna neno hata moja linalosemwa kuhusu [kuwa na mkutano wa] sala, sifa, au kuyasoma Maandiko.

Mfano wa tatu ulioandikwa, wakati mitume wale walipokusanyika siku ile ya Jumapili, unapatikana katika Matendo 2:1: "... [Mitume] walikuwako wote mahali pamoja." (Sikukuu ya



Pentekoste - Jumapili.) Basi, je! fungu hilo laweza kuwapatia ndugu zetu Wakristo hao wanaoifuata Biblia ishara ya kuwapa tumaini kwamba hapo Jumapili hatimaye inachukua mahali pa Jumamosi? Kwa maana sisi tunapowaambia kwamba Wayahudi walikuwa wameendelea kuitunza Jumapili hiyo kwa miaka 1500, na tena wamekuwa wakiitunza kwa karne kumi na nane [kufikia 1893] baada ya kuanzishwa Ukristo, na wakati uo huo wakiendelea kuitunza Sabato ya kila juma [Jumamosi], sisi hatuoni faraja yo yote au liwazo katika fungu hilo. Pentekoste ni siku ya hamsini baada ya Pasaka [2], ambayo iliitwa Sabato ya Majuma, ikiwa na siku saba mara saba; (na siku moja zaidi baada ya kumaliza siku ya Sabato ya kila juma ya juma lile la saba, ilikuwa ni siku kuu ya sikukuu zote, ikiwa ni Jumapili kwa kawaida. Ni Mwisraeli gani basi, ambaye asingeweza kusikitika kuiona kazi hiyo ya kujaribu kugundua chanzo cha [mwanzo wa] utunzaji wa siku ya kwanza ya juma kwa kuiangalia sikukuu yake ya Pentekoste, ambayo imetunzwa naye kwa zaidi ya miaka 3000? Ni nani kama siye yule Mkristo anayeifuata Biblia peke yake ambaye amegonga ukuta kwa kutafuta kisingizio cha kutoa udhuru wake kwa kuinajisi Sabato [Jumamosi], ambayo sikuzote ilishikwa na Kristo na mitume wake, ambaye angeweza kuigeukia sikukuu hiyo ya Kiyahudi ya Pentekoste ili kuutetea uasi wake dhidi ya Mungu na mwalimu wake, yaani, Biblia?

Mara moja tena, watetezi wa badiliko la siku hiyo wanaoifuata Biblia wanayageuzia mawazo yetu katika kitabu cha Matendo, sura ya 20, fungu la 6 na 7: "Hata siku ya kwanza ya juma [Jumapili], tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate,... n.k." Kwa mwonekano wote fungu hilo lililotajwa hapo juu lingeleta faraja kwa kiasi fulani kwa rafiki zetu wanaoifuata Biblia ambao hawajaridhika, lakini sisi tukiwa Waharabu wa hila yao, hatuwezi kuwaruhusu kupata hata makombo hayo ya mkate huo wa faraja. Tunajibu kwa kutumia maneno yasiyokanikika kabisa, tukisema: "Quod probat nimis, probat nihil" ----- "Kile kinachothibitisha kupita kiasi, hakithibitishi kitu cho chote." Hebu na tuyageuzie mawazo yetu kwa wazo lilo hilo katika Matendo 2:46: "Na siku zote [kila siku] kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu wakimega mkate nyumba kwa nyumba, n. k. Nani asiyeweza kuona mara moja kuwa fungu lile lililokwisha kutolewa ili kuthibitisha haki ya pekee ya Juma:pili [kuchukua mahali pa Jumamosi] linayeyuka na kupotea hewani ----- ni ignis fatuus ----- linapopambanishwa na fungu hili [la 46] la sura ile ile moja? Kile ambacho anadai Mkristo huyo anayeifuata Biblia kwa kutumia fungu hilo kumaanisha Jumapili peke yake kwa mamlaka [idhini] ile ile, Mtakatifu Luka anatupasha habari kwamba ilikuwa kila siku ya juma: "Na siku zote [kila siku] kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba."

Fungu moja zaidi hujitokeza lenyewe, likiwa na mwonekano wa kuiweka Jumapili mahali pa Jumamosi. Linadondolewa kutoka kwa Mtakatifu Paulo, 1 Wakorintho 16:1,2: "Kwa habari ya ile changizo [mchango, sio sadaka ya kawaida] kwa ajili ya watakatifu [wale walioko Yerusalemu - fungu la 3]." "Siku ya kwanza ya juma [Jumapili] kila mtu kwenu aweke akiba kwake [nyumbani kwake, sio kanisani]," n.k. Tuseme kwamba ombi lile la Mtakatifu Paulo lingekuwa limezingatiwa kwa makini, hebu na tuyageuzie mawazo yenu kwa kile kilichofanyika kila Jumamosi katika kipindi chote cha maisha ya Mwokozi na kuendelea kufanyika kwa miaka thelathini iliyofuata [baada ya kifo chake], kama kitabu cha Matendo kinavyotupasha habari.

Wafuasi wake Bwana walikutana "kila Sabato [Jumamosi]" kusikiliza Neno la Mungu; Maandiko yalisomwa "kila siku ya Sabato [Jumamosi]." "Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi [mazoea] yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya Maandiko kila Sabato [Jumamosi], n.k. Matendo 18:4 [17:2]. Ni hitimisho la kipuuzi jinsi gani kudhani kwamba kusoma Maandiko, kusali, kuonya, na kuhubiri, mambo ambayo yalikuwa ya kawaida kufanyika kila Jumamosi, kama

ilivyothibitishwa kwa namna ya kutosheleza sana, kuwa mambo hayo yote yaliamishwa katika siku ya Jumapili kutokana na ombi lile la kukusanya mchango katika siku nyingine ya juma?

Ili kupata manufaa kamili ya fungu hilo linalofikiriwa, ni jambo la maana kukumbushia kitendo kile walichofanya mitume na wanawake wale watakatifu siku ile ya Ijumaa Kuu kabla ya jua kuzama. Walinunua manukato na marhamu baada ya yeye [Kristo] kushushwa chini kutoka msalabani; wakaahirisha kufanya yote [yaliyotakiwa] mpaka Sabato "takatifu kwa Bwana" ilipokuwa imepita, hapo ndipo Jumapili alfajiri walipochukua hatua za kukikamilisha kitendo kile cha kuupaka mafuta mwili mtakatifu wa Yesu.

Twaweza kuuliza, Mbona hawakuikamilisha kazi ile ya kumpaka mafuta siku ile ya Jumamosi? --- -- Kwa sababu walijua fika kuwa kule kuupaka mafuta mwili mtakatifu wa Bwana wao kungeathiri utunzaji wa makini wa Sabato [Jumamosi], utunzaji ambao wao waliupa kipaumbele; na mpaka hapo itakaponyeshwa [vinginevyo] kuwa Siku ya Sabato [Jumamosi] ambayo ilikuwa imetangulia kabla ya Jumapili ya fungu letu hilo ilikuwa haijatunzwa (jambo ambalo lingekuwa ni uongo, kwa vile kila Sabato ilikuwa imetunzwa), ndipo ombi hilo la Mtakatifu Paulo la kukusanya mchango siku ya Jumapili likilinganishwa na fungu la kufanya kazi ya kuupaka mwili wa Kristo, ambayo isingeweza kufanyika siku ya Sabato [Jumamosi], na matokeo yake ni kwamba iliahirishwa mpaka siku ile ya pili ambayo ilionekana kuwa inafaa kwa kazi hiyo; yaani, Jumapili, au siku ya kwanza ya juma.

Baada ya kulishughulikia kila fungu linalopatikana katika Agano Jipya ambalo linaitaja Sabato (Jumamosi), na siku ile ya kwanza ya juma (Jumapili); na baada ya kutoa hitimisho thabiti kutokana na mafungu hayo, ambayo, mpaka hapo, hakuna hata kivuli kimoja cha kisingizio kinachoweza kupatikana katika Gombo hilo Takatifu [Biblia], kwa kuiweka Jumapili mahali pa Jumamosi kwa kufuata Biblia; basi, linalobakia kwetu ni kuchunguza maana ya usemi huu "Siku ya Bwana," na "Siku yake Bwana," unaopatikana katika Agano Jipya, jambo ambalo sisi tunakusudia kufanya katika makala yetu inayofuata, na kutoa hitimisho tukitoa maelezo ya maana dhidi ya mfumo huo wa dini usiofaa kitu ambao tutakuwa tumeuthibitisha kuwa hauwezi kutetewa, unajikanusha wenyewe, na kujifisha wenyewe.

---

Maelezo Chini ya Ukurasa Nyuma

[1] Kwa kweli sisi [Waadventista Wasabato] hatuyaungi mkono hata kidogo yale yanayosemwa hapa kumhusu Luther. Ni Walutheri peke yao wanaodhani kwamba Luther alikuwa na kweli yote, lakini kazi aliyofanya ilikuwa kubwa [na bora]. Alikuwa Mkristo shujaa. Laiti kama kazi yake ingeendelezwa mbele kama alivyoianza yeye, wafuasi hao wa papa wasingekuwa wanawafanyia mzaha "Waprotestanti" kwa kule kutokuwa na msimamo kwao kwa kukiri kuwa wao wanaikubali Biblia peke yake na wakati uo huo wakiwa wanafuata Mapokeo ya Kanisa Katoliki. ----- Mhariri.

[2] Pasaka daima ilikuwa siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza [wa Kiyahudi], bila kuitaja hata kidogo siku iwayo yote ya juma, na kwa hiyo ilikuwa haiwezekani kabisa kuwa sikuzote iwe ni "Jumapili kwa kawaida," kama ilivyoelezwa.

Maelezo haya yameingizwa tu kwa faida ya kuwa sahihi, sio kwa kusudi la kuwa yawe na uzito wo wote katika mabishano yaliyomo katika fungu hilo. ----- Mhariri.

---

[Toka katika Gazeti la Catholic Mirror la Sept. 23, 1893.]

"Kuchechemea juu ya magongo [milonjo] yasiyo na urefu unaolingana,  
Mguu mmoja ukiwa umeinuliwa juu kwa ile kweli, mmoja kwa uongo,  
Na hivyo kwenda kwa kuchechemea kuelekea kwenye goli lile,  
Hakuambui kitu cho chote isipokuwa kushindwa tu katika mbio hizo."

Katika makala hii ya sasa tunakusudia kuchunguza upya kwa makini (kundi lile la mwisho) la ushahidi ambao unafikiwa kuwa utamsadikisha Mkristo huyo anayeifuata Biblia ya kuwa Mungu alikuwa ameiweka Jumapili mahali pa Jumamosi kwa ibada yake katika Sheria mpya, na ya kwamba mapenzi ya Mungu yanaonekana yameandikwa na Roho Mtakatifu katika Maandiko ya mitume wale.

Tunaambiwa ya kwamba badiliko hilo kubwa limetajwa, tena na tena, katika mfululizo wa mafungu ambayo usemi huu, "Siku yake Bwana," au "Siku ya Bwana," unaweza kupatikana.

Katika Agano Jipya, tumelichunguza kundi la mafungu yapatayo sitini na moja hivi, chini ya kichwa cha "Sabato" katika vitabu vya Injili, Matendo, na Nyaraka; na kundi la pili, ambalo linaitaja "siku ya kwanza ya juma," au Jumapili, baada ya kuyachunguza kwa makini hayo ya kundi la mwisho yapatayo tisa [nane]; na kuyaona kuwa hayatoi kidokezo hata kidogo sana kuhusu badiliko la nia kwa upande wa Mungu kuhusu siku ile mwanadamu anayopaswa kumwabudu yeye [Mungu], sasa tunaendelea kuchunguza mafungu ya kundi la tatu na la mwisho yanayotumainiwa kuuokoa mfumo huo unaoitegemea Biblia ili isihukumu kwa hila yake ya kuupa ulimwengu, kwa jina la Mungu, amri hiyo [Jumapili] ambayo haina idhini hata kidogo au mamlaka kutoka kwa mwalimu wao, Biblia.

Fungu la kwanza katika kundi hili linapatikana katika Matendo ya Mitume 2:20: "Jua litageuka kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla ya kuja siku ile ya Bwana." Ni Jumapili ngapi zimepita tangu unabii huo ulipotolewa? Juhudi kubwa sana jinsi gani imetumika kuipotoa maana ya fungu hilo takatifu linalohusu siku ya hukumu ili liseme Jumapili!

Fungu la pili katika kundi hili linapatikana katika 1 Wakorintho 1:8: "Ambaye atawathibitisha hata mwisho, ili msilamiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo." Ni punguani [taahira] gani asiyeweza kuona kwamba hapo mtume huyo anaonyesha waziwazi siku ile ya hukumu? Fungu linalofuata katika kundi hili linalojileta lenyewe hupatikana katika Waraka uo huo, sura ya 5:5: "Kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu," Mkorintho huyo anayezini na mke wa babaye ndio kusema kweli kuwa aliokolewa Jumapili iliyofuata!! Hilo ni jambo la kusikitisha jinsi gani kuweka siku ya badala mahali hapo! Fungu la nne, 2 Wakorintho 1:13,14: "Nami nataraji ya kuwa mtayakiri hayo hata mwisho;... kama ninyi mlivyo kwetu sisi, katika siku ya ile ya Bwana wetu Yesu."

Je, hiyo ni Jumapili, au ni siku ya hukumu, ipi ni ipi? Fungu la tano linatoka kwa Paulo kwenda kwa Wafilipi, sura ya 1, fungu la 6: "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu." Watu wale wema wa Filipi katika kuufikia ukamilifu wao Jumapili iliyofuata, wangeweza kumudu kucheka kuliona badiliko hilo la haraka la siku hizi zetu!

Tunaomba ruhusa [kwenu ili tupate] kutoa, fungu letu la sita katika kundi hilo; yaani, Wafilipi, sura ya kwanza, fungu la kumi: "Ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo." Kwa hiyo siku ile ilikuwa Jumapili iliyofuata, je, ni kweli! basi, wasingengoja kwa muda mrefu vile. Fungu la saba, 2 Petro 3:10: "Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi [usiku]." Kulitumia fungu hilo kumaanisha Jumapili huvuka mipaka ya upumbavu.

Fungu la nane, 2 Petro 3:12: "Mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua," n.k. Siku hiyo ya Mungu ndiyo ile ile iliyotajwa katika fungu lililotangulia, matumizi ya mafungu yote hayo mawili yakimaanisha Jumapili iliyofuata yangeufanya ulimwengu ule wa Kikristo ukose usingizi kabisa siku ile iliyofuata ya Jumamosi usiku.

Tumekwisha kuwaonyesha wasomaji wetu mafungu nane kati ya tisa yanayotegemewa kuimarisha juhudi hiyo ya kukufuru kwa kutumia mafungu hayo na kuendeleza kwa hila "Siku ya Bwana" kwa kumaanisha Jumapili, na kwa matokeo gani basi? Kila moja [la mafungu hayo] hutupatia sisi ushahidi wa siku ile ya mwisho, yakiitaja moja kwa moja, kwa uthabiti kabisa, na bila kuwapo utata wo wote.

Fungu la tisa ambalo ndani yake tunaukuta usemi huo wa "Siku ya Bwana," ndilo la mwisho kuweza kupatikana katika Maandiko ya mitume wale. Kitabu cha Matukio ya Mwisho au Ufunuo, sura ya 1:10, hutueleza kwa maneno ya Yohana yafuatayo: "Nalikuwa katika Roho, Siku ya Bwana;" lakini halitaleta faraja nyingi zaidi kwa marafiki zetu hao wanaoifuata Biblia kuliko yale yaliyotangulia katika mfululizo huu. Je, Mtakatifu Yohana amepata kuutumia usemi huo huko nyuma katika Injili yake au Nyaraka zake. ----- Kwa nguvu, tunasema, Hapana. Je, alikuwa amepata kuitaja Jumapili wakati fulani huko nyuma kabla ya wakati huo? ----- Ndiyo, mara mbili. Je! aliipa cheo gani Jumapili katika matukio yale? Jumapili ya Pasaka iliitwa naye (Yohana 20:1) kuwa ni "siku ya kwanza ya juma."

Tena, katika sura ile ya ishirini, fungu la kumi na tisa, anasema: "Ikawa jioni, siku ile ya kwanza ya juma." Ni dhahiri kwamba japokuwa alikuwa amevuviwa alipoziandika Injili na Nyaraka zake, aliita Jumapili kuwa ni "siku ya kwanza ya juma." Kwa misingi gani, basi, inaweza kudhaniwa kuwa alikiacha cheo hicho [cha siu hiyo]? Je, alipata uvuvio mwingi zaidi alipokiandika kitabu kile cha Ufunuo, au alichagua cheo kingine kwa siku ya Jumapili, kwa sababu sasa alikuwa amezoea?

Jibu kwa mawali hayo lingekuwa limevuka mpaka katika jambo hili la mwisho, tukiona ya kwamba usemi ule ule ulikuwa umetumika mara nane tayari na Mtakatifu Luka, Mtakatifu Paulo, na Mtakatifu Petro, wote wakiwa chini ya uvuvio, na kwa hakika Roho Mtakatifu asingeweza kumvuvia Mtakatifu Yohana apate kuiita Jumapili kuwa ni Siku ya Bwana, wakati aliwavuvia Watakatifu Luka, Paulo, na Petro, wote kwa pamoja, kuipa cheo siku ile ya hukumu kuwa ni "Siku ya Bwana." Mabingwa wa lugha wanatambua miongoni mwa makusudi yakinifu yasiyoweza kukosea, kusudi moja la kimaadili la kutumia ulinganifu wa jambo linalohusika au kwa kutumia jambo linalojulikana ili lile lisilojulikana lipate kujulikana, ambalo kwalo sisi tunawezeshwa kuhitimisha jambo hilo kwa uhakika kwa kuangalia yanayojulikana na kwenda kwa yale yasiyojulikana; tukiwa na hakika kabisa kuhusu maana ya usemi ule ulionenwa mara nane, basi, sisi tunahitimisha tukisema kwamba usemi ule ule unaweza kuwa na maana ile ile moja tu unapoenwa kwa mara ya tisa, hasa tukijua kwamba katika matukio haya tisa semi zile zilikuwa zimevuviwa na Roho Mtakatifu.

Wala sababu zile za ndani zenye nguvu kabisa haziwezi kushindwa kuthibitisha kwamba (fungu) hili, kama mafungu yale mengine, lina maana ile ile moja. Mtakatifu Yohana (Ufu. 1:10) anasema: "Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana;" lakini anatupatia ufunguo wa usemi huo katika sura ile ya

nne, fungu la kwanza na la pili: "Baada ya hayo, naliona, na tazama, mlango ukafunguka mbinguni." Sauti ile ikamwambia hivi, "Panda hata huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo." Hebu kiroho tupande pamoja na Yohana. Wapi? ----- kupitia katika mlango [ule] mbinguni," na kuingia mbinguni. Je, tutaona nini kule? ----- "Mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo," sura ya nne, fungu lile la kwanza. Alipanda kiroho kwenda mbinguni. Aliamriwa kuandika kikamilifu, maono yake ya mambo yale ambayo yanapaswa kutokea kabla ya, na yale yanayoambatana na, "siku ya Bwana," au siku ile ya hukumu; usemi huo wa "Siku ya Bwana," katika Maandiko umehusishwa na siku ile ya hukumu peke yake.

Kwa bidii na usahihi tumekusanya katika Agano Jipya kila ushahidi unaoweza kupatikana ambao ungeweza kuthibitisha kwa kuikubali amri inayoifuta siku ya Sabato ya Sheria ile ya zamani [Amri Kumi], au ile inayoiweka siku nyingine [ya ibada] kwa kipindi hiki cha Ukristo. Tumekuwa waangalifu sana kubainisha kama tulivyofanya hapo juu, ili isije ikatolewa kauli ile isemayo kwamba Amri ile ya Tatu [1] ilifutwa chini ya Sheria Mpya. Hoja ya kujitetea kama hiyo imebatilishwa kwa kitendo cha Maaskofu wa Kanisa la Methodisti linaloongozwa na Maaskofu (Methodist Episcopal) katika Waraka wao wa kichungaji wa 1874, ulionukuliwa katika gazeti la New York Herald la tarehe ile ile, likiwa na sauti ifuatayo: "Sabato [Jumamosi] iliyowekwa mwanzoni na kuthibitishwa tena na tena na Musa na manabii, kamwe haijapata kufutiliwa mbali. Hiyo ni sehemu ya Sheria ile ya Maadili, wala hakuna sehemu yake au sehemu ndogo ya utakatifu wake ambayo imeondolewa." Tangazo hilo rasmi hapo juu limelifunga kundi hilo kubwa la Wakristo wanaoifuata Biblia kwa kuiweka amri ya tatu katika hali yake ya kudumu chini ya Sheria Mpya.

Tunaomba tena ruhusa ya kuyageuza mawazo ya wasomaji wetu kwa njia ya pekee kuiangalia kanuni ya ishirini ya "Kanuni Thelathini na Tisa za Dini" zilizomo katika Book of Common Prayer, isemayo hivi: "Si halali kwa Kanisa kuamuru jambo lo lote lililo kinyume na Neno la Mungu lililovuviwa."

## HITIMISHO

Katika mfululizo wa makala zetu hizi, tumekuwa waangalifu sana kwa ajili ya kuwaelimisha wasomaji wetu ili kuwaandaa kwa njia ya kuwapa idadi fulani ya kweli zisizokanushika ambazo zinapatikana katika Neno la Mungu ili kufikia hitimisho lisilokanushika kabisa. Mfumo huo unaoifuata Biblia ulipojitokeza katika karne ile ya kumi na sita, haukujinyakulia tu mali ya Kanisa [Katoliki], lakini katika vita yake ya kuharibu mambo kwa ujinga, kwa kadiri ulivyoweza, ukauvua Ukristo sakrameti zote zilizoanzishwa na Muasisi [Kanisa Katoliki], Misa, n. k., n.k. haukuacha kitu isipokuwa Biblia peke yake, ambayo wale waliokuwa wanaieleza wakaitangaza kuwa ni mwalimu wao wa pekee katika mafundisho na maadili ya Kikristo.

Kuu miongoni mwa kanuni zao za imani ilikuwa, na imekuwa mpaka leo hii, ile haja ya kudumu ya kuitakasa Sabato [Jumapili]. Kwa kweli, imekuwa kanuni ya imani ya pekee kwa miaka 300 iliyopita [kabla ya 1893] ambayo imekuwa kauli kamili ya wawakilishi hao wanaoifuata Biblia.

Kuitunza Sabato [Jumapili] hiyo ndiyo jumla na kiini cha nadharia yao ya kuifuata Biblia. Mimbara zao zinavuma kila juma kwa maneno mengi yasiyokoma ya makaripio dhidi ya ulegevu wa kuitunza Sabato [Jumapili] katika nchi zile za Kikatoliki, ikilinganishwa na utunzaji sahihi wa siku hiyo, yaani, wa Kikristo, ambao unajitosheleza wenyewe katika nchi zile zinazoifuata Biblia. Ni nani awezaye kusahau hasira kali takatifu inayodhihirishwa na wahubiri hao wanaoifuata Biblia katika mapana na marefu ya nchi yetu hii, kutoka katika kila mimbara ya Kiprotestanti, kwa kadiri hoja hiyo ya kuifungua Sikukuu ya Ulimwengu ya Tamasha na Kuuza Vitu katika siku ya Jumapili ilivyokuwa haijaamuliwa; na ni nani asiyejua siku hizi, kuwa dhehebu moja, kuonyesha ghadhabu yake takatifu dhidi ya maamuzi yaliyotolewa, halijayafungua kabisa masanduku yake ambayo yalikuwa na bidhaa zao mahali pale ilipofanyika Sikukuu hiyo ya Ulimwengu ya Tamasha na Kuuza Vitu?

Wakristo hao wazuri kabisa, wasemaji wenye nguvu, kwa kuchunguza sana Biblia yao kwa makini, wanaweza kuwapata wenzi wao katika kundi fulani la watu wasio wema wa siku zile za Mkombozi wetu, waliomwendea mara kwa mara usiku na mchana, wakiwa wameudhika kupita kiasi, na kufedheheshwa kupita uwezo wao wa kustahimili, kwa kuwa hakuitunza Sabato [Jumamosi] kwa njia iliyonyooka kama wao wenyewe walivyoitunza.

Walimchukia kwa kutumia akili yake kuhusiana na siku ile, naye hakuweza kupata maneno ya kutosha kuelezea dharau nyingi kabisa aliyokuwa nayo kwao kwa kiburi chao cha Kifarisayo. Na yawezekana sana kwamba mawazo ya Mungu hayajafanya mabadiliko katika mtazamo wake leo dhidi ya makelele makubwa ya wafuasi wao na wale wanaowaunga mkono mwisho wa karne hii ya kumi na tisa. Lakini tunapoyajumlisha yote ukweli ni kwamba Mafarisayo wale wa zamani wakati wao walikuwa wanaitunza Sabato ya kweli [Jumamosi], Mafarisayo wetu wa siku hizi, tukiuchukulia ujinga wao wa kuamini bila kuwa na ushahidi na udanganyifu wao wa kijinga, katika maisha yao hawajapata hata mara moja kuitunza Sabato ya kweli [Jumamosi] ambayo Bwana wao wa mbinguni aliitunza mpaka siku ya kufa kwake, na mitume wake waliitunza, kufuata kielelezo chake, kwa miaka thelathini baadaye, kwa mujibu wa Kumbukumbu hiyo Takatifu [Biblia], tofauti inayoonekana wazi kwa watu wote, inahusu kukataa kwa kukufuru kwa makusudi amri ile inayopaswa kutekelezwa kabisa, jambo hilo huonekana kwetu katika kitendo cha Ulimwengu huo wa Kikristo unaoifuata Biblia. Biblia na Sabato [Jumapili] ndilo neno kuu la Uprotestanti; lakini sisi tumeonyesha kuwa ni Biblia dhidi ya Sabato yao [Jumapili]. Tumekwisha kuonyesha kuwa hakuna tofauti kubwa iliyopata kuwako kuliko nadharia na desturi yao hiyo. Tumethibitisha kwamba si babu zao wa zamani walioifuata Biblia, wala wao wenyewe waliopata kuitunza hata Sabato [Jumamosi] moja katika maisha yao.

Waisraeli na Waadventista Wasabato (Seventh-day Adventists) ni mashahidi wa kitendo chao [Waprotestanti hao] cha kuinajisi siku ile iliyotajwa na Mungu kwa kurudia tena na tena, na wakati ambapo wao wamempuuzwa na kumhukumu mwalimu wao, yaani, Biblia, wameichagua siku ile inayotunzwa na Kanisa Katoliki. Ni Mprotestanti gani baada ya kusoma kwa makini makala hizi tulizozitoa, kwa dhamiri safi, atakayeendelea kuivunja amri ya Mungu, inayomwamuru kuitunza Jumamosi, amri ambayo mwalimu wake, yaani, Biblia, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo anaandika kuwa hayo ndiyo mapenzi ya Mungu kwetu sisi?

Historia ya ulimwengu haiwezi kuonyesha mfano wa kijinga, unaopumbazisha akili kama huo wa kosa la kuacha kufanya kulingana na kanuni inavyotaka. Mwalimu huyo katika kila ukurasa

unaoitaja Amri ya Sabato [Jumamosi] anadai kwa nguvu kuwa itunzwe kila juma na wale wote wanaomtambua kuwa yeye ndiye "mwalimu wao asiyekosea kamwe," ambapo wafuasi wa mwalimu huyo kwa zaidi ya miaka mia tatu [kufikia 1893] hawajapata kuitii amri hiyo ya Mungu hata kwa mara moja tu! Mkutano ule mkuu wa Wakristo wale wanaoifuata Biblia, yaani, Wamethodisti, wametangaza ya kwamba Sabato haijapata kamwe kufutiliwa mbali, ambapo wafuasi wa Kanisa la Anglikana, pamoja na binti yao, yaani, Kanisa Linaloongozwa na Maaskofu la Marekani (Episcopal Church of U.S.A.) wamefungwa, kwa kanuni hiyo ya ishirini ya dini yao ambayo tayari imekwisha kutajwa, kwa sheria ile isemayo kwamba Kanisa haliwezi kuamuru kihalali jambo lo lote lililo "kinyume na Neno la Mungu lililoandikwa." Neno la Mungu lililoandikwa linaamuru kwa hakika, tena na tena, na kwa mkazo kwamba ibada inapaswa kufanywa siku ya Jumamosi, linatoa tishio la waziwazi la kuuawa yule asiyetii. Madhehebu zote zinazoifuata Biblia zinakalia msimamo uo huo unaopumbaza akili ambao hakuna maelezo yo yote yawezayo kuugeza au kwa uchache wake kuhalalisha.

Ni kwa kweli ilioje maneno yale ya Roho Mtakatifu yanatumika kwa hali hiyo ya kusikitisha sana! "Iniquitas mentita est sibi." ----- "Uovu umejiongoepa wenyewe." Wakidai kuwa wanaifuata Biblia peke yake kama mwalimu wao, lakini mbele ya ulimwengu, mwalimu huyo wa pekee [Biblia] anatupiliwa kando kwa njia ya kufedhehesha sana, na mafundisho na desturi ya Kanisa Katoliki ---- - "mama wa machukizo yote," kama inafaa kwa makusudi yao kumwita hivyo ----- wanayachagua hayo, licha ya matishio yanayoogofya sana yaliyotamkwa na Mungu mwenyewe dhidi ya wale wasioitii amri ile isemayo, "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase."

Kabla ya kuufunga mfululizo wa makala hizi, tunawasihi wasomaji wetu kuyageuzia mawazo yao mara moja tena kwenye maelezo yetu yale ya utangulizi, yanayoingiza kila hoja; kama vile, 1. Sabato ya Kikristo [Jumapili], ni mtoto halali wa muungano wa Roho Mtakatifu pamoja na Kanisa Katoliki kama bibi-arusi wake. 2. Madai ya Waprotestanti kwa sehemu yo yote ile katika hoja hii yamethibitishwa kuwa hayana msingi, yanajikanusha yenyewe, na kujifisha yenyewe.

Azimio la kwanza linahitaji ushahidi kidogo sana. Kanisa Katoliki kwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya kuwako Mprotestanti mmoja, kutokana na utume wake liliopewa na Mungu, liliibadili siku [ya ibada] kutoka Jumamosi kwenda Jumapili. Tunasema kutokana na utume wake liliopewa na Mungu kwa sababu yule aliyejiita mwenyewe kuwa ni "Bwana wa Sabato," alilipa uwezo wake mwenyewe wa kufundisha, akisema, "awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi" [Luka 10:16]; aliwaamuru wote wanaomwamini yeye kulisikiliza kanisa, kwa tishio la adhabu ya kuwekwa katika fungu moja na "mataifa na watoza ushuru"; tena aliahidi kuwa pamoja nalo mpaka mwisho wa dahari [ulimwengu]. Linashikilia hati yake itokayo kwake ----- hati isiyoweza kukosea kamwe ambayo ni ya milele. Ulimwengu wa Kiprotestanti wakati ule wa kuzaliwa kwake uliikuta Sabato hiyo ya Kikristo [Jumapili] ikiwa imejizatiti kwa nguvu mno kiasi cha wao kutoweza kuiondoa ili isiwepo; kwa hiyo, ukajikuta umo katika hali ya kulazimika kuafikiana na mpangilio huo, ikimaanisha hivyo kuwa Kanisa [Katoliki] lina haki ya kuibadili siku hiyo kwa zaidi ya miaka mia tatu mpaka sasa [1893]. Kwa hiyo, Sabato hiyo ya Kikristo [Jumapili] mpaka siku hii ya leo, inatambuliwa kuwa ni mtoto wa [imeanzishwa na] Kanisa Katoliki kama bibi-arusi wa Roho Mtakatifu, bila kuwako neno hata moja la kutugombeza kutoka kwa Ulimwengu huo wa Kiprotestanti.



Lakini, hebu sasa na tuangalie kwa haraka tu azimio letu la pili, tukiwa na Biblia peke yake kama mwalimu na kiongozi katika mambo yale yahusuyo imani na maadili. Mwalimu, huyu anakataza kwa nguvu kabisa kufanya badiliko lo lote la siku kwa sababu zenye maana sana. Amri hiyo [ya Sabato (Jumamosi)] inataka liwepo "agano la milele." Siku hiyo linayoamriwa kutunzwa na mwalimu huyo [Biblia] haijapata kamwe kutunzwa nao hata mara moja, hivyo wameanzisha uasi wao dhidi ya kanuni hiyo iliyokazwa, na kuonekana kwamba wanajikanusha wenyewe, wanajipumbazisha akili wenyewe, na hatimaye kujiangamiza wenyewe kama uwezo wetu wa kujieleza kwa maneno unaweza kuruhusu kusema hivyo.

Wala mipaka ya uhalifu wao haijafikiwa bado. Mbali na hiyo. Unafiki wao kwa kukiacha kifua cha Kanisa Katoliki ulikuwa ni ukengefu [uasi] kwa kuiacha ile kweli kama inavyofundishwa katika neno hilo lililoandikwa. Walilichagua Neno lililoandikwa kama, ndilo mwalimu wao wa pekee, ambaye mara tu walipompokea wakamwacha kwa ghafula, kama makala zetu hizi zilivyothibitisha kwa kiasi kikubwa; na kwa upotovu wao ulio wa makusudi kama vile ulivyo na makosa, wanalikubali fundisho la Kanisa Katoliki wakipingana ana kwa ana na mafundisho yaliyo wazi, yasiyobadilika, na ya kudumu ya mwalimu wao wa pekee katika fundisho hilo la maana sana la dini yao, kwa njia hiyo kuikaza hali yao ambayoi naweza kuitwa vyema kuwa ni ya "kudhihakiwa, ya udanganyifu, na mtego."

---

[MAELEZO YA MHARIRI. ----- Ni kwa hoja iyo hiyo Matengenezo ya Kanisa (Reformation) yalishutumiwa na Baraza la Trenti. Wanamatengenezo ya Kanisa walikuwa wametoa mashtaka ya kudumu, kama yalivyoenezwa humu, kwamba Kanisa Katoliki lilikuwa limeasi kutoka katika kweli kama ilivyo katika neno hilo lililoandikwa. "Neno lililoandikwa," "Biblia na Biblia peke yake," "Hivyo ndivyo asemavyo Bwana," haya yalikuwa ndiyo maneno yao makuu; na "Maandiko kama yalivyo katika Neno lililoandikwa, ndiyo kanuni ya pekee ya madai," hilo ndilo jukwaa lililotangazwa la Matengenezo ya Kanisa na Uprotestanti. "Maandiko na mapokeo." "Biblia kama ilivyotafsiriwa na Kanisa [Katoliki] na kwa kufuata kibali chao cha pamoja cha wale Mababa," huo ndio ulikuwa msimamo na madai ya Kanisa Katoliki. Hiyo ndiyo ilikuwa hoja kuu katika Baraza lile la Trenti, ambalo liliitishwa kwa madhumuni hasa ya kujadili hoja zilizokuwa zimetolewa na kulazimishwa kuingia katika mawazo ya watu wa Ulaya kwa njia ya Wanamatengenezo wale. Hoja ya kwanza kabisa kuhusu imani iliyojadiliwa na baraza lile ni hoja iliyotajwa katika toleo la kijitabu hiki. Kulikuwa na kundi lenye nguvu hata miongoni mwa Wakatoliki katika baraza lile waliopendelea kuachilia mbali mapokeo na kutumia Maandiko peke yake kama kanuni ya mamlaka. Maoni hayo yalishikiliwa kwa uthabiti katika mijadala ya baraza lile hata wawakilishi wale wa papa wakamwandikia wakimweleza kwamba "palikuwapo na mwelekeo wenye nguvu katika kuyaweka kando kabisa mapokeo na kuyafanya Maandiko kuwa ndiyo kanuni pekee ya madai." Lakini kufanya hivyo kungekuwa ni kwenda mbali sana na kuyahalalisha madai ya Waprotestanti. Kutokana na mgogoro huo kilianzishwa kikundi kilichokuwa na msimamo mkali wa Kikatoliki, kikijaribu kufanya kazi ya kuwashawishi wale wengine kuwa "Maandiko na mapokeo" ulikuwa ndio msingi pekee, wa hakika wa kusimama juu yake. Kama jambo hilo lingeweza

kufanyika, basi, baraza lile lingeongozwa kutoa tangazo linaloyashutumu Matengenezo yale ya Kanisa, vinginevyo lisingeweza kufanya hivyo. Hoja hiyo ilijadiliwa siku kwa siku, mpaka baraza lote likafikia mahali pa kukaa kimya. Hatimaye, baada ya maumivu mengi ya muda mrefu na makubwa ya kutumia akili, Askofu Mkuu wa Reggio akaingia ndani ya baraza lile kimsingi akiwa na sababu ifuatayo kwa kundi lile lililoshikilia Maandiko peke yake:

"Waprotestanti wanadai kusimama juu na neno lile lililoandikwa peke yake. Wanakiri kuyashikilia Maandiko peke yake kama kanuni yao ya imani. Wanahalalisha maasi yao kwa dai kwamba Kanisa [Katoliki] limeliyasi neno lile lililoandikwa na kwamba linafuata mapokeo. Basi, madai hayo ya Waprotestanti kuwa wanasimama juu ya neno lililoandikwa peke yake si ya kweli. Madai yao ya kuyashikilia Maandiko peke yake kama ndiyo kanuni ya imani ni ya uongo. Ushahidi: Neno lile lililoandikwa linaamuru utunzaji wa siku ya saba [Jumamosi] kama ndiyo Sabato yenyewe. Wao hawaitunzi siku ya saba [Jumamosi], bali wanaikataa. Kama kweli wanayashikilia Maandiko peke yake kama kanuni yao, basi, wangukuwa wanaitunza siku ya saba [Jumamosi] kama ilivyoamriwa katika Maandiko yote. Lakini si kwamba tu wanaukataa utunzaji wa Sabato hiyo [Jumamosi] iliyoamriwa katika neno hilo lililoandikwa, bali wamechagua na wanaendelea kuitunza Jumapili, ambayo imejengwa tu juu ya mapokeo ya Kanisa [Katoliki]. Matokeo yake ni kwamba dai hilo la 'Maandiko peke yake kama ndiyo kanuni, limeshindwa; na fundisho hili la dini la 'Maandiko na mapokeo' kuwa vyote ni muhimu, limejiimarisha sana, Waprotestanti wenyewe wakiwa waamuzi."

Hapakuwa na njia yo yote ya kulikwepa hilo, kwa maana usemi wa Waprotestanti wenyewe wa kuthibitisha imani yao ----- yaani, Ungamo la Augsburg, 1530 (the Augsburg Confession, 1530) --- -- kwa wazi kabisa lilikuwa limekiri kuwaw "utunzaji wa Siku ya Bwana [Jumapili]" ulikuwa umechaguliwa na "Kanisa" peke yake [sio kwa misingi ya Biblia].

Sababu hiyo ilishangiliwa katika baraza lile wakisema inatokana na uvuvio peke yake; kundi lile la "Maandiko peke yake," likajisalimisha; na baraza lile mara moja likawashutumu Waprotestanti kwa kauli moja na Matengenezo yale yote ya Kanisa kuwa ni uasi usiotakiwa kutoka katika usharika na mamlaka ya Kanisa Katoliki; na Aprili 8, 1546 likaendelea "kutoa matangazo mawili, la kwanza linalotoa amri, kwa tishio la laana (anathema), isemayo kwamba Maandiko na mapokeo yanapaswa kupokewa yote mawili na kupewa heshima sawa, na ya kwamba vitabu vile vya Maandiko ya Siri (Apokrifa) ambavyo havikupitishwa kuwa Maandiko Matakatifu ni sehemu ya Maandiko hayo yaliyokwisha kukubaliwa. Amri ya pili ikatangaza kwamba Toleo la Biblia kwa lugha ya Kilatini (Vulgate) ndilo toleo la kweli na la kutumika na wote, na kulipa mamlaka kuwa linakuwa badala ya maandiko yale ya asili; ikikataza kutafsiri Maandiko kinyume cha mawazo yaliyotolewa na Kanisa [Katoliki], 'au hata kinyume cha kauli ya pamoja ya Mababa wale,' " n.k. [2].

Hivyo basi, ulikuwa ni msimamo wa Kiprotestanti unaolegalega katika desturi zao uliolipa Kanisa Katoliki sababu yao iliyotafutwa kwa muda mrefu na kwa shauku kubwa ili kuushutumu Uprotestanti na tapo [kundi] lote lile la Matengenezo ya Kanisa kuwa ni uasi unaotokana na sababu za kibinafsi za kujitafutia makuu dhidi ya mamlaka ya Kanisa [Katoliki]. Na katika mabishano hayo ya maana sana ufunguo, uliokuwa mkuu mno na wenye kufikia kilele chake wa kulegalega kwa msimamo wa Waprotestanti ulikuwa ni ule wa kuikataa Sabato ya Bwana, yaani, siku ya saba, ambayo Maandiko yameamuru, na badala yake kuchagua kuitunza Jumapili kama ilivyoamriwa na Kanisa Katoliki.

Na mpaka leo hii huo ndio msimamo wa makundi hayo mawili katika mabishano hayo. Leo, kama hati hii inavyoonyesha, hiyo ndiyo hoja ya maana sana ambayo Kanisa Katoliki inatumia kuuhukumu Uprotestanti, na ambayo juu yake Kanisa hilo linashutumu njia iliyochaguliwa na Uprotestanti unaopendwa na wengi kuwa "haiwezi kutetewa, inajikanusha yenyewe, na kujifisha yenyewe." Waprotestanti hao, na Uprotestanti huo, watafanyaje?]

---

Waheshimiwa wachungaji hao, waliozoea kupiga makelele sana juu ya sababu ya kweli au ya kudhaniwa tu dhidi ya kuinajisi siku ile takatifu ya udanganyifu [Jumapili], yaani, [ile wanayoifikiria kuwa ni] Sabato ya Biblia, kama wangefikiria vyema kuleta ukinzani wao dhidi ya uchambuzi wetu huu wa busara na uliojengwa juu ya Maandiko uliokikatakata vipande vipande kinyama chao wanachokipenda sana [Jumapili], basi, sisi tunaweza kuwapa ahadi kwamba jaribio lo lote la maana kwa upande wao la kukusanya vipande vipande vilivyokataliwa (dissecta membra) vya kinyama chao hicho kilichozalishwa na wazazi wawili, na kukirejeshea uhai uliotiwa nguvu ya umeme, sisi tutakutana nao kwa urafiki wa kweli na kuwafikiria kwa heshima kwa upande wetu.

Lakini tunaweza kuwahakikishia wasomaji wetu ya kuwa tunawajua vizuri mno hao wanaopiga kelele sana kuweza kutazamia kubwata kwa mara moja kutoka kwao katika jambo hili. Nao wanatujua vizuri mno kuweza kujitia chini ya uchambuzi wetu unaowafedhehesha ambao tungeongeza juu ya huu ili kuwakatakata vipande vipande juu ya hoja hii [Jumapili] isiyoungwa mkono na Maandiko. Siasa yao sasa ni "kulala chini," tena ni hakika wataitumia.

---

## MAELEZO CHINI YA UKURASA NYUMA

1. Kwa hesabu za Kikatoliki, Amri ile ya Sabato ni ya tatu miongoni mwa zile Amri

Kumi.

2. Angalia mambo yaliyojadiliwa katika Baraza lile; Ungamo la Augsburg; na

Ensaiklopedia Britannica, makala "Trent, Council of."

## NYONGEZA I

---

Makala hizi zimechapishwa tena, na kijitabu hiki kimetolewa kwenu na wachapishaji, kwa sababu kinatoa kutoka katika chanzo kisichoweza kukanushwa na kwa sauti ya hakika, awamu ya hivi karibuni ya mabishano juu ya utunzaji wa Jumapili, ambayo sasa, na ambayo kwa kweli kwa muda fulani, yamekuwa sio tu hoja ya kitaifa katika mataifa makuu, bali pia yamekuwa kama hoja ya kimataifa. Si kwamba sisi tunafurahia kuona mambo yakiwa hivyo; tungependa mambo hayo yangekuwa vinginevyo. Tungependa kwamba Waprotestanti kila mahali wawe na msimamo thabiti kabisa katika imani na desturi yao hata isiwepo nafasi ya kuwapo uhusiano kati yao na Roma kiasi cha kuchukua sura uliuochukua hivi sasa.

Lakini hali katika jambo hili kwa sasa ni kama ilivyoielezwa humu. Hatuwezi kuukwepa ukweli huu. Kwa hiyo, ni jukumu la Chama cha Kimataifa cha Uhuru wa Dini kutangaza kwa mapana kadiri iwezekanavyo sura halisi ya hoja hii kuu kama ilivyo hivi sasa. Si kwa sababu tunafurahia kuona ikiwa hivyo, bali kwa sababu ndivyo ilivyo, haidhuru sisi au mtu mwingine ye yote ange au asisngefurahia mambo kuwa hivyo.

Ni kweli kwamba tumekuwa tukiiangalia hoja hiyo kwa miaka mingi ili ipate kuchukua hali yake halisi iliyo nayo sasa, ambayo imeelezwa waziwazi katika kijitabu hiki. Tumewaambia watu tena na tena, na hasa Waprotestanti na hata hivyo, tumewaambia wale waliokuwa wanatetea kuanzishwa kisheria kwa Jumapili katika Marekani, kwamba katika njia ile waliyokuwa wanaifuata walikuwa wakicheza moja kwa moja mikononi mwa Roma, na ya kwamba kufanikiwa kwao kwa hakika [katika hoja hii], kungewafanya bila kukwepa kuitwa na Roma, na Roma ikijipatia uwezo pia, ingeweza kuwapasha habari kwa nini Jumapili hiyo ingepaswa kutunzwa. Jambo hilo tumewaambia watu kwa miaka mingi kwamba litakuja hakika. Na sasa kwa kuwa limekuja, ni jukumu letu kulitangaza tu ili watu wajue kwa mapana yake yote kadiri itakavyokuwa katika uwezo wetu kufanya hivyo.

Huenda swali likaulizwa, Kwa nini Roma hakujitokeza kwa nguvu mapema kama anavyofanya sasa? Kwa nini alingoja kwa muda mrefu mno? Haikuwa kwa manufaa yake kufanya hivyo mapema. Wakati atakapofanya kazi yake, alitaka aifanye akiwa na nguvu [mamlaka], na nguvu hiyo mpaka sasa alikuwa hanayo. Lakini katika jitihada yao kubwa sana ili wapate kutambuliwa na taifa na serikali ya Marekani na kuwekwa kwa [amri ya] Jumapili, Waprotestanti wa Marekani walikuwa wanamfanyia kazi zaidi yeye [Roma] kuliko vile ambavyo yeye angeweza kujifanyia kwa njia ya kujipatia mamlaka ya kiserikali mikononi mwake. Hayo alijua sana, na kwa hiyo alingojea tu. Na sasa kwa vile Waprotestanti, wakiungana naye, wametekeleza jambo hilo la kuogofya sana, mara moja yeye anainuka kwa kiburi chake chote cha asili na roho ile ya wakati ule wa zamani, na kuwaamuru Waprotestanti kutoa jibu kwake kwa utunzaji wao wa Jumapili. Hili nalo anafanya pia kwa sababu yeye yu salama katika mamlaka ambayo Waprotestanti kwa upofu wao wameyaweka mikononi mwake. Kwa maneno mengine, uwezo ambao Waprotestanti wameuweka mikononi mwake sasa atautumia kwa maangamizi yao. Je, unahitajika ushahidi mwingine wo wote kuonyesha kwamba gazeti hilo la Catholic Mirror (ambalo linamaanisha Kadinali yule na Kanisa Katoliki la Amerika) lilikuwa linangojea fursa kama hiyo, kuliko ule uliotolewa katika ukurasa wa 17 wa kijitabu hiki? Tafadhali rudi nyuma na kuangalia ukurasa ule na kuona kwamba dondoo lililotolewa katika gazeti la New York Herald, mwaka ule wa 1874, limeletwa sasa mbele yenu kwa njia hiyo. Je hilo halionyeshi waziwazi kuwa usemi ule wa Maaskofu Wamethodisti, na gazeti hilo la Mirror, kwa miaka yote hiyo kumi na tisa, wameyatunza mpaka kwa wakati kama huu? Na zaidi ya hayo, Waprotestanti watkutana na mambo zaidi kama hayo ambayo yamehifadhiwa [na Roma], ambayo yatatumika kwa njia ambayo itawashtua na kuwafanya wawezi kuchanganyikiwa.

Wakati huu wa sasa hilo ndilo zogo kati ya Kanisa Katoliki na Waprotestanti. Mambo yakiwa hivyo, basi, sisi tunatoa tu uhariri huu kwa gazeti lile la Catholic Mirror. Pointi zile zinazobishaniwa ndizo pointi zinazodaiwa na Waprotestanti kuwa zinawaunga mkono. Hoja imetolewa na Kanisa Katoliki; jibu linawakalia Waprotestanti wale wanaoitunza Jumapili, sio juu yetu sisi [tunaoitunza Jumamosi]. Kwa kweli tunaweza kusema hivi, "Hayo si mazishi yanayotuhusu sisi." Kama hawajibu, basi, [Roma] atafanya ukimya wao kuwa ni kukiri kwao kwamba yeye ana haki kufanya hivyo alivyofanya, naye atawatendea ipasavyo. Kama watajibu, basi, atayatumia maneno yao wenyewe dhidi yao, na kama nafasi itaruhusu wakati itakapohitajika, atautumia uwezo ule waliouweka mikononi mwake. Kwa kadiri yeye [Roma] anavyohusika, kama Waprotestanti wanajibu au hawajibu, ni mambo kwake. Na jinsi anavyowaangalia na roho ile aliyo nayo katika kuwashughulikia kuanzia sasa na kuendelea imeonyeshwa waziwazi katika changamoto iliyotolewa katika aya ya mwisho ya makala hizi zilizochapishwa tena. Kimbilio ni moja tu lililobaki kwa Waprotestanti. Yaani, kwamba wanapaswa kuchukua msimamo wao thabiti na kwa ukamilifu kusimama juu ya "neni lililoandikwa peke yake," "Biblia na Biblia peke yake," na hivyo kusimama juu ya Sabato yake Bwana [Jumamosi]. Hivyo wakiwa hawaikubali mamlaka yo yote ila ile yake [Bwana] (Eze. 20:12,20), wakiitii Amri yake hiyo, na kulindwa kwa uwezo wake, hapo ndipo watakapopata ushindi juu ya Roma na washirika wake wote, na [hatimaye] kusimama juu ya bahari ile ya kioo, wakiwa na vinubi vya Mungu, ambavyo kwa hivyo wataherehekea ushindi wao mkuu milele hata milele. (Ufunuo 18, na 15:2-40).

Waprotestanti hao hawajachelewa mno kujikomboa wenyewe. Je! watafanya hivyo? Je, watakuwa na msimamo thabiti kuitetea imani hiyo ya Kiprotestanti? au wataendelea kukalia hali yao hiyo

"isiyoweza kutetewa, inayojikanusha yenyewe, na kujifisha yenyewe" ya kujidai ni Waprotestanti wakati bado wanasimama juu ya uwanja wa Kikatoliki, wakipokea matusi kutoka kwa Wakatoliki, na kustahimili shutuma za Wakatoliki? Je! kweli watalishikilia neno peke yake, yaani, Maandiko peke yake kama ndiyo mamlaka yao ya pekee na kanuni yao ya pekee? au bado wataendelea kushikilia fundisho lao na desturi yao hiyo "isiyoweza kutetewa, inayojikanusha yenyewe, na kujifisha yenyewe kwa kufuata mamlaka ya Kanisa Katoliki na kuivaa ishara ya mamlaka yake [Jumapili]? Je! wataweza kuitunza Sabato ya Bwana [Jumamosi], yaani, siku ya saba, kwa mujibu wa Maandiko hayo? au wataitunza Jumapili kwa mujibu wa mapokeo ya Kanisa Katoliki?

Mpendwa msomaji, wewe utachagua kufanya lipi?

## NYONGEZA II

---

Tangu toleo lile la kwanza la kijitabu hiki lilipochapishwa, yafuatayo yalitokea katika safu ya uhariri ya gazeti lile la Catholic Mirror, la Desemba 23, 1893:

"Kwa shauku kuu ambayo uhariri wetu huu umetafutwa, na kuonekana tena katika uchapishaji uliofanywa na Chama cha Kimataifa cha Uhuru wa Dini (International Religious Liberty Association), uliochapishwa kule Chicago, wenye kichwa hiki cha 'Changamoto Toka Roma: Kwa Nini Waprotestanti Wanaitunza Jumapili?' ambalo liliuzwa kule Chicago, New York, California, Tennessee, London, Australia, Cape Town, Afrika, na Ontario, Canada, pamoja na hitaji kubwa

linaloendelea kutoka kwa watu, limefanya iwe lazima kwa gazeti hili la Mirror kuyapa mfumo wake wa kudumu, na hivyo kukidhi hitaji hilo.

"Kurasa za kijitabu hiki humfunulia msomaji mojawapo ya ukinzani wa wazi usioweza kufikirika uliopo kati ya desturi na nadharia ya Ulimwengu huo wa Kiprotestanti, na usioelekea kusuluhishwa kwa kutumia busara iwayo yote ile, nadharia yao ile inayodai kwamba Biblia peke yake ndiye mwalimu wao, ambaye bila utata wo wote na kwa nguvu kabisa anaamuru Jumamosi 'itakaswe,' ambapo desturi yao inathibitisha kwamba wanayapuuzia kabisa matakwa ya mwalimu wao huyo, yaani, Biblia, na kufuata sababu ya Wakatoliki kwa karne tatu na nusu [kufikia 1893], kwa kuiacha nadharia yao hiyo, wanasimama mbele ya ulimwengu leo wakiuwakilisha mfumo wa dini usioweza kabisa kutetewa, unaojikanusha wenyewe, na naojifisha wenyewe unaoweza kuwaziwa.

"Tunajisikia kwamba hatuwezi kuwafurahisha wasomaji wetu zaidi kuliko kutoa 'Nyongeza' hii [1] ambayo Chama cha Kimataifa cha Uhuru wa Dini, Shirika la Kiprotestanti lenye msimamo mkali, kiliyaongeza kwenye makala zetu tulizotoa. Kuisoma kwa makini nyongeza hiyo kutathibitisha ukweli kwamba hoja yetu tuliyotoa humo haijibiki, na ya kwamba njia peke yake iliyobaki kwa Waprotestanti hao ni aidha kuondoka katika eneo la Kikatoliki ambalo wamelikalia kwa karne tatu na nusu [kufikia 1893], na kumkubali mwalimu wao, yaani, Biblia, kwa imani safi, kama alivyoshauri waziwazi mwandishi wa Nyongeza hiyo kwamba waanze mara moja kuitunza Jumamosi, siku ambayo Biblia inaamuru kuwa itunzwe kuanzia Mwanzo mpaka Ufunuo; au, waiachilie mbali Biblia kama mwalimu wao wa pekee waache kukaa katika eneo letu bila ruhusa yetu, na kuwa wakinzani hai wa kanuni zao wenyewe, kisha wapokee barua [kutoka kwetu] za kufanywa wana wa ufalme wa Kristo duniani ----- yaani, Kanisa lake [Katoliki] -----wasiendeleo kuteseka tena wakijidanganya wenyewe na kujikanusha wenyewe.

"Hoja zilizotolewa katika kijitabu hiki zimejengwa imara juu ya neno la Mungu, na zikiwa zimefanyiwa utafiti wa karibu sana, Biblia ikiwa mkononi, haziachi mwanya wo wote wa kutorokea kwa Mprotestanti mwenye bidii isipokuwa kuiacha kwake ibada hiyo ya Jumapili na kurudia ile ya Jumamosi, iliyoamriwa na mwalimu wao, Biblia, au, kama hataki kuachana na mapokeo ya Kanisa Katoliki, linaloamuru utunzaji wa Jumapili, jambo ambalo wamelikubali kwa kumpinga ana kwa ana mwalimu wao, Biblia, basi, kwa uthabiti ayapokee mafundisho yake yote [ya Kikatoliki]. Sababu na kutumia akili hulazimisha kuukubali upande mmoja au ule mwingine katika mambo haya mawili ya kuchagua: ama Uprotestanti na kuitakasa Jumamosi, ama Ukatoliki na kuitunza Jumapili. Kusimama katikati ni jambo lisilowezekana kabisa."



